

Eastern Africa Journal of Kiswahili

[ISSN 2958-1036]
Volume: 01 Issue: 01 | July-2022

EAJK

# Usawiri wa mandhari kibibliotherapia katika hadithi fupi teule za Kiswahili

**Authors**
**Rose Mavisi[(1)]; Wendo Nabea[(2)]**
**Main author email:** rosemasai@gmail.com

**(1.2) Laikipia University, Kenya.**

**Cite this article in APA**
Mavisi, R. & Wendo, N. (2022). Usawiri wa mandhari kibibliotherapia katika hadithi fupi teule za Kiswahili. *Eastern Africa journal of Kiswahili*, 1(1), 33-42. https://doi.org/10.51317/eajk.v4i1.137

OPEN ACCESS A publication of Editon Consortium Publishing (online)

**Article history**
Received: 15.07.2022
Accepted: 16.07.2022
Published: 24.07.2022

Scan this QR to read the paper online

**Copyright:** ©2022 by the author(s). This article is an open access article distributed under the license of the Creative Commons Attribution (CC BY NC SA) and their terms and conditions.

**Ikisiri**
Mandhari huwa ni sehemu muhimu katika kazi ya Sanaa. Mtunzi hutumia mandhari kuibua maudhui na sifa za wahusika. Mandhari ni mahali au makazi maalum yaliyojengwa na mtunzi na mnamotukia matukio mbalimbali ya kazi ya fasihi. Makala haya yalilenga kupambanua sifa za kibibliotherapia katika mandhari ya diwani teule za hadithi fupi za Kiswahili. Diwani hizo ni zifuatazo; *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* (2004), *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* (2007), *Kiti cha Moyoni na Hadithi Nyingine* (2007) na *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine* (2016). Utafiti huu ulifanywa maktabani ambapo data ziliweza kukusanywa kwa kutumia mbinu ya udurusu wa vitabu. Mtafiti alipitia maandishi mbalimbali kutoka katika vitabu teule vya hadithi fupi pamoja na wavuti ili kupata maelezo yaliyotosha kukidhi haja ya Makala haya. Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Mapatano ya Mwitikio wa Msomaji (NMMM) yake Rosenblatt (1995) ili kumsaidia mtafiti kupambanua sifa za kibibliotherapia katika mandhari. Matokeo ya utafiti huu yalibaini kwamba bibliotherapia hujitokeza katika mandhari yanayosawiriwa katika diwani hizi za hadithi fupi teule.

**Maneno muhimu:** Mandhari, bibliotherapia, hadithi fupi.

**UTANGULIZI**

Wamitila (2003), anasema kuwa mandhari hutumiwa kueleza sehemu ambako tendo fulani hutendeka. Neno hili huweza kutumika kwa mapana kueleza pia mazingira ya kiteknolojia ya tendo fulani. Anaongeza kusema kuwa mandhari yana nafasi na umuhimu mkubwa katika hadithi fupi, na kwamba ni lazima msomaji ajitahidi kuangalia kama kuna uhusiano kati ya mandhari na vipengele vingine vya utunzi kama wahusika, dhamira, maudhui, ujumbe na kadhalika. Wamitila (khj) anahoji kuwa mazingira huweza kuwa ya kijamii, kitamaduni, kisasa, kihistoria na kadhalika. Njogu na Chimerah (1999) wanakubaliana na haya wanaposema kuwa ni mazingira ya wahusika pamoja na matukio na inahusu mahali wanamokaa wahusika na kuingiliana. Mazingira haya ni ya kiuchumi na ya kijamii ya wahusika hao na nafasi zao za kitabaka. Hata hivyo mandhari ya hadithi fupi huwa finyu.

**MAPITIO YA MAANDISHI**

Hadithi fupi ni mojawapo ya vigeu tulivyovitazama katika utafiti huu. Hadithi fupi ni miongoni mwa tanzu zinazosomwa na wanafunzi wa shule za upili katika somo la fasihi. Wamitila (2002), anaeleza kuwa, ubanifu ndio sifa ya kimsingi katika hadithi fupi. Ubanifu wa hadithi fupi humfanya mwandishi asitoke nje ya mada lengwa. Mwandishi wa hadithi fupi hulazimika kuwakuza wahusika wake waonekane kama wahusika waliokuzwa kikamilifu kisifa na kitabia. Mtunzi wa hadithi fupi hulazimika kujifunga kwenye mada kuu. Kimandhari na kimaudhui lazima ubanifu ujitokeze. Aidha hadithi fupi haitarajiwi kutumia mbinu rejeshi kwa upana kwa sababu ya wakati uliotengewa uundaji wa msuko. Ufupi unaoelezwa hapa ni ile hali inayomsukuma mtunzi kuteua mbinu za kimtindo, lugha na mpangilio zitakazomwezesha kueleza machache kwa njia ya kibanifu. McOnyango (2006) anahoji kuwa utanzu wa hadithi fupi ulizuka miaka sitini iliyopita. Habwe (2010) naye anadai kuwa hadithi fupi imejitokeza kama njia kuu ya kuarifu, kuliwaza, kushauri na kuelekeza watu katika jamiii nyingi. Anaongeza kusema kuwa hadithi fupi huweza kushughulikia jambo lolote mradi linasibu maisha ya binadamu.

Wanafunzi walizisoma hadithi fupi teule na kubainisha ikiwa sifa za BB zilijitokeza. Bibliotherapia ni mbinu muhimu inayoweza kutumiwa kama kipumuo kwa vijana kwa baadhi ya matatizo yanayowakumba katika kipindi fulani cha maisha yao. Bibliotherapia humsaidia msomaji kupitia mtagusano wake na mandhari, maudhui na wahusika ambao wamepitia hali kama ya yule msomaji. Hata hivyo, kuna mwongozo wa kufuata wakati wa uteuzi wa kitabu kwa matumizi ya bibliotherapia. Wataalamu ambao wameshughulikia kipengele cha bibliotherapia kama Kavanaugh na Fiorini (2009), miongoni mwa wengine, wamependekeza sifa zifuatazo kuzingatiwa katika uteuzi wa vitabu vinavyotumika kwa bibliotherapia: Kitabu kilichoteuliwa kinahitaji kuwa na hadithi inayovutia. Tatizo na suluhisho linaloshughulikiwa linahitaji kuaminika. Pia, mhusika mkuu awe kielelezo bora. Mwanafunzi asifadhaishwe na kuumizwa na mambo fulani katika kitabu hicho na aweze kujitambulisha na mhusika mkuu. Hadithi ilenge umri wa mwanafunzi na iweze kupokelewa na tamaduni mbalimbali huku ikizingatia usawa wa kijinsia. Mandhari ya hadithi fupi yanafaa kuwa sifa hizi zitatoa mwelekeo katika uteuzi wa vitabu vya kusomwa na wanafunzi kwa matumizi ya BB.

Mwasisi wa nadharia hii ni Rosenblatt (1995). Mwitikio ni mwendelezo wa ushirikiano baina ya mtu binafsi na kazi ya fasihi. Ushirikiano huu unaweza kuendelea kwa muda hata baada ya mtu kumaliza kukisoma kitabu. Mwitikio unaweza kujitokeza kupitia kazi zinazopendwa au zinazokataliwa. Katika nadharia hii, kitendo cha usomaji ni muhimu sana. Carlisle (2000), aliendelea kueleza kuwa nadharia hii husisitiza jukumu la ubunifu wa msomaji. Alisisitiza umuhimu wa hali ya usemezano kati ya msomaji na matini. Naye Rosenblatt (1995), alifafanua nadharia hii kama mwingiliano wa msomaji na matini ya fasihi katika ubadilishaji ambao huathiri na kubadilisha matini na kuathiri maana.

Rosenblatt (1995) amegawa miitikio ya msomaji katika vitengo viwili: Kwanza, kuna mwitikio wa kiujumi ambapo msomaji anaposoma matini, hujumuisha mambo kama vile kufikiria, kuhisi na kupata tajriba ya kifasihi kutokana na kazi anayoisoma. Aina hii ya mapatano hulenga hali ya kutambua jinsi vipengele tofauti vya kifasihi kama vile uhusika, fani na maudhui huingiliana na kuchangia katika kukuza ukamilifu wa kazi ya kifasihi. Pili, kuna mwitikio wa kieferenti, ambapo unasisitiza ufahamu wa habari asilia. Lengo kuu huwa ni kuyapata maarifa au maadili fulani baada

ya kuzisoma kazi za kifasihi. Mtafiti katika utafiti huu aliegemea miitikio yote miwili ambayo iliwafaa wanafunzi walipozisoma hadithi fupi teule. Njia hizi mbili za usomaji hukamilishana

**MATOKEO**

**Mandhari na BB katika Hadithi Fupi Teule**

Mtafiti katika kazi hii aliangazia mandhari ya hadithi fupi kwa mtazamo wa kibibliotherapia. Kwa mujibu wa Kavanaugh na Fiorini (2009), wamependekeza sifa zifuatazo kuzingatiwa katika usawiri wa mandhari kibibliotherapia. Kwanza mandhari yawe na uhalisia na yaweze kuaminika na yaangazie tajriba za wanafunzi wa shule za upili kwa mujibu wa utafiti huu. Sifa hizi zilimfaa mtafiti kuweza kupambanua mandhari kibibliotherapia katika hadithi fupi teule.

**a) Mandhari ya Shuleni na BB**

Waandishi katika baadhi ya hadithi wamesawiri mandhari ya shuleni. Katika hadithi ya *Kanda la Usufi* katika diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi* Nyingine, kuna mandhari ya shuleni. Wahusika Sela na Masazu ni wanafunzi wa shule ya upili. Mwandishi anasema;

> *Sela alikuwa mwanafunzi katika shule ya bweni ya Askofu Timotheo. Masazu kwa jina jingine Chris alikuwa mwanafunzi wa shule ya upili ya Lenga Juu. Shule mbalimbali katika eneo la Mlimani zilikuwa zikishiriki tamasha ya muziki katika shule hiyo ya wasichana. Uk. 137.*

Mandhari ya shuleni vile vile yanajitokeza katika hadithi fupi ya *Ndimi za Mauti* katika diwani ya *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine.* Mwandishi anasawiri shule ya upili ya Angeko. Katika shule hii kuna wanafunzi watatu ambao walipanga mgomo wa kuchoma shule hivyo kusababisha vifo vya wenzao. Mwandishi anasema;

> *Vijana watatu walipenyeza huku na huku na kutokeza kwenye upembe mmoja uliotwaliwa na vazi zito la giza totoro. Eneo zima la shule lilikuwa kimya; hapasikiki chochote isipokuwa sauti dhaifu za*
> *kereng'ende. Taa zote zilikuwa zimezimwa Uk 125.*

Vile vile, katika hadithi fupi ya *Fumbo la Mwana* katika diwani hiyo ya *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine*, mwandishi amesawiri mandhari ya shuleni. Mhusika Nanda ni mwanafunzi wa shule ya upili. Mwandishi anasema;

> *Mwalimu mkuu alimweleza jinsi Nanda alivyobadilika pakubwa kwa muda usiozidi muhula mmoja. Alimweleza jinsi ambavyo Nanda anafika shuleni aghalabu akiwa amechelewa siku hizi….Uk. 93.*

Mwalimu mkuu alimhitaji mzee Atanasi kufika pale shuleni ili kuzungumzia kuhusu mabadiliko ya Nanda kitabia pale shuleni.

Nayo hadithi fupi ya *Mtihani wa Maisha* katika diwani ya *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine,* mandhari ya shuleni yamesawiriwa. Mwandishi anasema;

> *Samuel alipita katika baraste inayoelekea kwenye lango kuu la shule. Wanafunzi ambao ndio mwanzo wamemaliza kipindi cha mwisho cha alasiri wamesambaa hapa na pale kwenye kiambo cha shule…Uk. 134.*

Katika hadithi fupi hizi tatu, mandhari ya shule yalijitokeza bayana. Mandhari ya shule husawiri hali halisi katika maisha ya wanafunzi na huweza kuaminika, hivyo kuzua BB kwa mwanafunzi. Katika hadithi ya *Kanda la Usufi*, mandhari ya shuleni yanasawiri hali halisi ya maisha ya kila siku ya wanafunzi. Mandhari yanayosawiri hali halisi huwa na sifa za kibibliotherapia. Sela ni mwanafunzi wa shule ya Askofu Timotheo ilhali Masazu ni wa Lenga Juu. Wote wanapatikana katika mandhari ya shule wakati wa tamasha za muziki za eneo la Mlimani. Naye Nanda katika hadithi ya *Fumbo la Mwana* na Samuel katika *Mtihani wa Maisha* wote wamesawiriwa katika mandhari ya shule. Kwa mujibu wa Rosenblatt (1978), katika nadharia ya NMMM, hadhira hubashiri na kuyahusisha wayakutayo katika hadithi na yale aliyoshuhudia maishani. Mwanafunzi anaposoma hadithi hii, anakuwa katika nafasi bora ya kuihusisha na shule yake. Wanafunzi wanaposoma hadithi kama hii, wao hutagusana na mandhari halisi ya shule ambayo wamekutana nayo katika maisha yao. Mandhari ya BB sharti yaaminike kwa wanafunzi (Maich na Kean, 2004). Kujitambulisha na mandhari katika hadithi huwa ndio mwanzo wa bibliotherapia. Mandhari huibua maudhui ya kazi husika na kuwasaidia wahusika kukuza sifa na tabia zao.

**b) Mandhari ya Usiku na BB**

Wamitila (2003) akirejelea mandhari ya wakati, anasema kuwa dhana hii hutumika kurejelea kipindi ambacho hali na matukio yanayosimuliwa na uwasilishaji wake hutokea. Wamitila (khj) anadai kuwa kuna wakati hadithi. Huu ni muda ambao huchukuliwa na kisa kinaposimuliwa.Wakati katika hadithi unaweza kukisiwa au uwe umetajwa katika kisa chenyewe. Vile vile, matumizi ya nyakati mbalimbali yanaweza kutusaidia kutambua wakati mahususi wa hadithi. Hata kama hadithi nyingi huandikwa kwa kutumia wakati uliopita, dhamira yake hulenga wakati uliopo.

Mtafiti alibaini kuwa kuna mandhari ya usiku katika diwani za hadithi fupi hizi. Katika jamii nyingi za Kiafrika, kuna imani kwamba matendo maovu hutendeka usiku. Mandhari ya usiku yamesawiriwa kwa sababu ni sehemu ya maisha ya jamii. Wanafunzi wengi hutagusana na usiku maishani mwao ila inawabidi kuwa waangalifu. Katika hadithi fupi ya *Mame Bakari* katika diwani ya *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine,* mwandishi anasema:

> *Sara anaikumbuka vyema siku ile. Ilikuwa saa tatu unusu usiku. Alikuwa akirudi darasa la ziada. Wenyewe waliziita 'twisheni'. Kila sehemu ya ule ukanda wa picha alikuwa akiikumbuka kasoro machache tu. Aliyaona hivi yakiingiliwa na kuharibiwa. Ujauzito wa kubakwa na kulazimishwa…*
> *Uk. 47.*

Mandhari ya usiku yalichangia kwa mhusika Sara kubakwa na kupata ujauzito. Hii ni hali halisi na inayoaminika katika jamii ya wanafunzi. Vile vile, hadithi fupi ya *Nipe Nikupe* katika diwani ya *Kiti cha Moyoni na Hadithi ningine.*
Vitushi vya hadithi hii vinatendeka usiku. Mwandishi anaangazia ukahaba katika mandhari haya.
Anasema;

> *Mzee Machua alipowasili usiku wa manane kwenye Baeyi Resort Club na Lexus lake lililokuwa na fahari ya kubeba kisichana kichanga, hakuna aliyegutuka. Wagutuke nini na huo ndio mtindo? Uk. 143.*

Vile vile, katika hadithi fupi ya *Koinange Usiku* katika diwani ya *Kiti cha Moyoni na Hadithi Nyingine,* mwandishi anasawiri hali halisi ya maisha katika barabara ya Koinange wakati wa usiku. Ripota wa Kalima TV yuko hiari kuanika uozo unaojitokeza pale. Anasema;

> *Boss nataka kukusanya habari kuhusu viroja vya Koinange usiku Uk. 166.*

Katika hadithi ya *Mkimbizi* katika diwani ya *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine,* mwandishi amesawiri mandhari ya usiku kuonyesha mashambulizi yaliyotokea nchini Rwanda kati ya Wahutu na Watutsi hasa wakati wa usiku. Msimulizi anasema;

> *Tulikuwa tukikaa kijijini Rugitare. Hapo usiku mmoja tulisika bunduki zikipiga. Baba alionekana mbabaifu. Ninakumbuka usiku uliotangulia huo baba na mwenzake walikuwa wakizungumza juu ya mzozo baina ya Wahutu na Watutsi… Usiku wa kwanza na hasa baada ya wiki moja nyumba yetu ilishambuliwa. Uk 116*

Msimulizi alieleza jinsi hivi vitendo vya kijambazi vilitendeka wakati wa usiku. Majambazi hupenda kujificha gizani ili wasionekane. Mandhari ya usiku yaliibua maudhui ya dhuluma.
Hadithi ya *Maeko* katika diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* ina mandhari ya usiku ambapo mhusika Duni hurudi kutoka vikao vya ulevi akiwa chakari huku akiimba wakati wenzake wamelala. Mwandishi anasema,

> *Ulikuwa ni usiku wa mkubwa. Yapata saa saba na nusu. Ingawa mbalamwezi iling'ara kwa juhudi zote mtaa wa Sebleni ulikuwa umegubikwa na utulivu mkuu. Kimya! Sauti ndogo tu ya mchakarisho wa paka atafutaye riziki katika madebe ya taka, ingeliweza kusafiri mitaa kadhaa kwa mapana na marefu. Usiambe kelele za mtiribu huyu aliyekwishalewa chakari Uk. 50.*

Waandishi wa hadithi hizi wamesawiri mandhari ya usiku. Haya ni mandhari yanayoaminika kwa wanafunzi hivyo kuzua bibliotherapia kwao. Mandhari ni kipengele kinachobanwa katika hadithi fupi. Mandhari ya hadithi fupi hayatarajiwi kuwa mapana na yaliyochukua muda mrefu. Sehemu ndogo ya kijiografia na muda mdogo wa kiwakati unaweza kutosha kuwasilisha dhamira ya mwandishi. Waandishi hawa wanaonyesha maovu yanayotendeka wakati wa usiku. Kuna ukahaba unaoendelea pale barabara ya Koinange.Vile vile, katika hadithi ya *Nipe Nikupe,* hata jizee la Mzee Machua linajikosea heshima na kuwa na

uhusiano na vitoto vidogo. Anatumia mali kama sumaku ya kuwavuta. Mandhari haya ya usiku yanawafunza wanafunzi maadili ya kujiepusha na kutembea usiku. Maich na Kean (2004) kupitia mwongozo wao, wanasema kuwa mandhari inayofunza maadili huzua bibliotherapia kwa wanafunzi. Vilevile, kupitia hadithi fupi ya *Maeko,* wanafunzi wanajifunza kujiepusha na ulevi. Kwa mujibu wa Carlisle (2000), katika nadharia ya NMMM, usomaji ni mfanyiko na humbadilisha msomaji. Mwanafunzi anaposoma hadithi hizi, matarajio yetu ni kuwa mtazamo wake kuhusu masuala yaliyotajwa utabadilika. Hata hivyo, watunzi wanafaa kuwa waangalifu kuhusu matumizi ya mandhari ya madanguro na vilabu vya vileo kwani yanaweza kukwaza bibliotherapia.

**c) Mandhari ya Asubuhi na BB**

Katika hadithi ya *Fumbo la Mwana katika diwani ya Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine,* mwandishi amesawiri mandhari ya mchana kupitia kwa wahusika wake. Nanda anamletea babake barua iliyomhitaji kwenda kumuona mwalimu shuleni kwa sababu mwanawe Nanda alikuwa ameanza kubadilika kitabia na kuwa mlegevu kimasomo. Ilibidi mzee Atanasi kwenda pale mchana. Mwandishi anasema;

> *Katika ile barua, mwalimu mkuu alimtaka mzee Atanasi afike huko shuleni keshoye saa tatu unusu hivi, wajadiliane kumhusu mwanawe Uk. 91.*

Mandhari ya asubuhi ni mwafaka kwa sababu masomo shuleni huanza saa mbili asubuhi hadi saa kumi jioni. Mandhari haya yatasaidia kuibua maudhui katika hadithi fupi husika. Vile vile, katika hadithi fupi ya *Msamaria Mwema* katika diwani ya *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine,* mwandishi amesawiri mandhari ya asubuhi. Mhusika Likono alikuwa anajiandaa kufika pale kanisani kwa sababu ilikuwa ni siku ya Jumapili. Mwandishi anasema;

> *Jua ndio kwanza linajitahidi kutokeza nyuma ya mawingu yaliyotanda angani Uk. 78.*

Siku ya Jumapili waumini wa kikristo hufika kanisani mapema kuhudhuria ibada. Likono alikuwa mmoja wao. Mandhari ya asubuhi yanajitokeza katika hadithi fupi ya *Kanda la Usufi* katika diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*. Matukio haya yalijitokeza katika shule ya Askofu Timotheo. Kila asubuhi, wanafunzi walijumuika gwarideni kabla ya masomo kuanza. Mwandishi anasema;

> *Jumatatu ya juma la tatu la muhula ilianza kama siku nyingine. Wanafunzi walijumuika gwarideni. Maombi ya asubuhi yalifanywa. Mwalimu wa zamu aliwakumbusha wanafunzi majukumu yao… Uk. 62.*

Mandhari ya asubuhi yalitoa nafasi kwa walimu kuweza kuwashauri na kuwaelekeza wanafunzi wote wa shule. Pili, ilitoa nafasi ya wanafunzi kuweza kusali pamoja kabla ya kuanza shughuli za siku. Mandhari haya ni halisia kwa wanafunzi wa shule, hivyo huweza kuzua bibliotherapia. Wanaposoma zile hadithi fupi, watayaamini mandhari haya.

**d) Mandhari ya Vyuoni na BB**

Mandhari ya vyuoni husawiri mazingira au mahali ambapo wanafunzi wa vyuo vikuu husomea. Katika hadithi fupi ya *Samaki wa Nchi za Joto katika diwani ya Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine,* mandhari ya chuo kikuu yanasawiriwa hasa kupitia Chuo Kikuu cha Makerere nchini Uganda. Mhusika Christine anakiri kuwa;

> *Zac tulisoma naye Chuo Kikuu cha Makerere. Wakati huo chuo hiki kilipagazwa jina la 'Harvard ya Afrika.'uk 11*

Vilevile, katika hadithi fupi ya *Damu Nyeusi* katika diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine,* mwandishi amesawiri mandhari ya chuo kikuu. Mhusika Fikirini alikuwa mwanafunzi wa chuo kikuu kimoja kule ughaibuni. Mwandishi anasema:

> *Basi lilimuacha… akisubiri karibu na mtaa alikopangisha chumba kuenda darasani chuoni… Fikirini aliamua kuanza kutembea au sivyo akose masomo siku hiyo. Chuoni si karibu lakini likija basi lingine… Uk. 22.*

Nayo hadithi ya *Mapenzi ya Kifaurongo* katika diwani ya *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine,* mwandishi anazungumzia mandhari ya chuo kikuu. Katika chuo hiki, Penina na Dennis ni miongoni mwa wanafunzi. Mwandishi anasema;

> *Dkt Mabonga yumo ukumbini anatoa mhadhara wa somo la Fasihi. Ukumbi huo wa mhadhara una wanafunzi wapatao mia moja Uk. 12.* Mhusika Dennis anasisitiza akiwazungumzia wanafunzi wenzake: *Sikosei*

> *kamwe nisemapo kwamba kuja kwao katika Chuo Kikuu cha Kivukoni kunastahiki……Uk. 13.*

Mtafiti alibaini kuwa mandhari ya vyuo viku yana uhalisia kwa wanafunzi. Kupitia hadithi fupi ya *Samaki wa Nchi za Joto,* kuna wanafunzi kama Christine ambao wanapuuza kisomo na kuingilia anasa. Kupitia mandhari, maudhui huweza kujitokeza na hata sifa na tabia za wahusika kama Christine. Katika hadithi ya *Mapenzi ya Kifaurongo,* tunamwona Dkt Mabonga akiwa darasani akifunza somo la fasihi. Ufunzaji ni mojawapo ya shughuli katika chuo kikuu. Mandhari ya vyuoni yanaaminika kwa wanafunzi, hivyo kuzua bibliotherapia kwa wanafunzi wa shule za upili. Kavanaugh na Fiorini (2009) wamependekeza kuwa kitabu kilichoteuliwa kwa bibliotherapia kinahitaji kuwa na hadithi inayoaminika. Kitabu kinachoaminika sharti kiwe na mandhari ya kuaminika kama haya ya vyuoni.

**e) Mandhari ya Mashambani na BB**

Mandhari ya mashambani yamesawiriwa kwa baadhi ya diwani za hadithi fupi teule. Katika hadithi ya *Kachukua Hatua Nyingine* katika diwani ya *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine,* mwandishi amesawiri mandhari ya mashambani. Mavitu alimshauri mkewe Sakina kuiacha kazi ya ualimu mjini ili aende kijijini kuendeleza kazi ya kilimo. Mwandishi anasema kumhusu Sakina;

> *Aliiacha kazi na kuanza kushughulikia kazi ya kupanda mboga, maharage na mahindi na mazao mengine…uk42*

Miaka miwili baadaye, Mavitu alichukua hatua ya pili. Aliamua kuacha kazi ya kuuza cherehani huko mjini na kuja kijijini kupanda mahindi na maharage pamoja na mkewe. Mandhari haya ni ya mashambani. Vile vile, katika hadithi fupi ya *Kikaza* katika *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine,* mwandishi anasema;

> *Mawingu mazito meusi yalionekana kutanda kote….wanakijiji. Walijitahidi kuviweka vitu aina aina mahali pazuri. Mahindi yaliwekwa ghalani. Mtama ukatiwa maguniani…Uk 41.*

Hawa wanakijiji walikuwa wakitarajia mvua kubwa kunyesha ndipo walijitahidi kuweka vitu vyao mahali pazuri. Hadithi imesawiri jamii ambayo hushiriki kilimo na ufugaji. Wao hutegemea mvua katika shughuli zao za kilimo. Mvua ikikosekana au kuchelewa maisha ya wanakijiji huwa hatarini. Katika hadithi fupi ya *Siku ya Mganga* katika diwani ya *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine,* mganga Mwaibale na familia yake waliishi kijini na ilikuwa nadra wao kufika mjini. Wakati mganga alipofika aliajabia aliyoyaona pale jijini. Mwandishi anasema;

> *Mwaibale alikuwa amejitenga mbali mno na maeneo waliyokuwa wakiishi binadamu wengine. Masomo pekee waliyokuwa wakiyafahamu wanawe yalikuwa yale ya kulima, kuchunga mifugo na kumsaidia baba yao katika shughuli za uganga Uk. 21.*

*Katika hadithi fupi ya Mke Wangu katika diwani ya Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine,* mwandishi amesawiri aina mbili za matabaka. Kwa upande wa tabaka la chini waliishi sehemu ambazo si za kutajika kama vile mashambani. Aidha, hawakutarajia kutangamana na watu wa tabaka la juu. Kila wakati walituhumu na kuchukuliwa kuwa hawakupaswa kwenda katika maeneo ya makazi ya watu matajiri ila pale walipohitajika kuwatumikia. Kwa hivyo kazi za sulubu na ngumu zilifanywa na tabaka hili. Kazi za kuchoma mihogo, ukulima, kuangua na kuuza madafu. Mandhari yanayosawiriwa katika hadithi hii ni ya uhalisia katika jamii. Wanafunzi katika jamii huweza kutagusana na mandhari kama haya. Wengine huishi katika mandhari husika hivyo kuaminika.

Mandhari ya mashambani huwa ni halisi hivyo kuweza kuzua bibliotherapia kwa wanafunzi. Baadhi ya wanafunzi huishi katika mazingira haya kwa hivyo wanaposoma vitabu vilivyo na mandhari haya, huzua bibliotherapia. Mwanafunzi huileta tajriba yake katika kazi husika anapoisoma. Rosenblatt (1995) anasema kuwa msomaji huja na dhana, amali na imani ambazo huthibitishwa na yale anayokutana nayo katika kazi ya fasihi.

**f) Mandhari ya Madongoporomoka na BB**

Mandhari ya Madongoporoma huwasawiri watu walio katika hali ya umaskini.

Mwandishi katika hadithi fupi ya *Ndoa ya Samani* katika diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* amesawiri wahusika wanaoishi katika mandhari ya kimaskini.

Katika kijiji cha msimulizi kuna watu ambao hawakujiweza kimaisha. Anasema;

> *Kijijini kwetu tulikuwa maskini waliokuwa wakipigiwa mfano. Hakuna aliyekuwa na uwezo wa kumuauni mwenzake Uk. 86*

Posa ya msimulizi inakataliwa kwa sababu alikuwa ni maskini. Vile vile, katika hadithi fupi ya *Tumbo Lisiloshiba* katika diwani ya *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine,* itikadi ya wakubwa ilishikilia kuwa jiji halikuwa na nafasi tena kwa hivyo walianza mikakati ya kuichukua ardhi ya wanyonge. Kiongozi alisema;

> *Na ardhi yenyewe iko wapi basi? Labda Madongoporomoka ndiko ardhi ilikobaki- kule wanakoishi watu wepesi wasio na mashiko. Kunakoishi watu wasiojua hadhi na faida za ardhi… Kunako mashonde ya vinyeshi…kunako vibanda uchwara vinavyozungukwa na uozo na bubujiko la maji machafu uk 4.*

Mandhari haya yanaonyesha hali halisi katika jamii hasa jinsi viongozi huwanyanyasa wachochole kwa kutaka kuchukua ardhi yao kule Madongoporomoka. Bi Suruta kudai kuwa vizito wenye fedha wana njama ya kunyakua shamba la wanyonge. Mandhari haya yanaweza kutumika kwa bibliotherapia kwa sababu yanaaminika.

Katika hadithi fupi ya *Ndoto ya Mashaka* katika diwani ya *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine,* mhusika Mashaka anaishi katika hali ya uchochole. Mandhari ya hadithi hii yanasawiri hali halisi. Ujenzi wa nyumba katika kitongoji hiki hauna mpangilio maalum. Kwa mfano, makazi ya Mashaka kule Tandale yamekumbatiana na choo cha jirani kwa hivyo harufu ya choo hiki huingia kwenye chumba chao. Maji yanayotumiwa na wakazi wa hapa humwagwa katika mto Msimbazi. Wao hutumia choo cha karatasi na nyumba zao zimeezekwa kwa madebe. Msimulizi anathibitisha haya asemapo;

> *Nyumba yetu nzuri kuiangalia kwa nje. Ina paa la madebe yaliyopiga rangi ya chuma. Ishara ya kuchoka labda. Na yenyewe hayajifichi kila msimu wa mvua ukifika. Husema kwa vitendo kuwa yamechoka kazi. Utayaona yakimwaga michirizi ya maji kama chekeche! Uk. 75*

Anaendelea kusema;

> *Aidha chumba hicho hakikuwa na vitu vingi. Kwanza tungevinunulia nini? Mshahara wenyewe mkia wa mbuzi! Na pili vingekaa wapi? Na sisi tungechutamia wapi? Hakikuwa na meza wala kiti. Hakikuwa na kitanda wala godoro…Uk. 76*

Katika hadithi ya *Maskini Babu Yangu* katika diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*, mwandishi amesawiri mandhari ya Madongoporomoka. Baadhi ya mitaa kama vile Daando, Summa na Kochokocho imesawiriwa katika hali ya kukatisha tamaa.

> *Mitaa hiyo ilijulikana kwa kashfa yaani Madongoporomoka…Uk. 77*

Mwandishi akizungumzia makazi haya ya madongoporomoka alitoa kauli ifuatayo;

> *Taswira hii ya mazingira ya mnuko usiostahimilika, mnuko ulioweza kuripua pua, ingali kichwani hadi sasa. Uk. 78*

Mandhari ya makazi ya hadithi hizi yanasawiri hali halisi ya Madongoporomoka. Hadith fupi hizi zinaweza kutumiwa kwa bibliotherapia. Kwa mujibu wa Njogu na Chimerah (1999), mandhari pia hutupa mwelekeo kuhusu maudhui. Hadhira hubashiri na kuyahusisha wayakutayo katika hadithi na yale waliyoshuhudia maishani. Wanafunzi wanaposoma HF hizi, wao huleta tajriba zao, uzoefu wao wa zamani, imani, matarajio na mawazo vilevile kuingiliana na mitazamo katika matini. (Rosenblatt, 1995)

**g) Mandhari ya Mjini na BB**

Katika hadithi fupi ya *Damu Nyeusi* katika diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi* Nyingine, mwandishi alikusudia kuyahusisha pia mandhari ya Afrika Mashariki kwa namna ya kipekee. Mandhari yanabanwa kwa ustadi wa hali kwa kutaja tu baadhi ya vitu vinavyoiwakilisha Afrika Mashariki, hasa ametaja miji. Kwa mfano; mwandishi anasema:

> *Alikumbuka siku zake za fahari alipofuatia warangi kwenye kitongoji cha Kibuye jijini **Kampala,** gongo kwenye vichochoro vya Ubungo, **Dar es Salaam** na chang'aa kwenye fondogoo la Mathare, **Nairobi**" Uk. 22*

Hapo ametaja maeneo matatu ya miji mikuu ya nchi tatu za Afrika Mashariki kwa lengo la kuiwakilisha Afrika Mashariki na watu wake. Hali kadhalika, katika sehemu nyingine anasema;

> *Alikumbuka dada zake kutoka kanda ya ziwa miongoni mwa Wahaya aliokutana nao alipokuwa anasomea ualimu katika Chuo cha **Walimu cha Mwanza**. Alikumbuka dada zake Wanyankole alipowahi kuzuru **Uganda-Magharibi**. Alikumbuka dada zake. Wakamba alipokutana nao alipokwenda ziara **Kitui** Uk. 24.*

Katika hadithi fupi ya *Gilasi ya Mwisho Makaburini* katika diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine,* mandhari yanayosawiriwa ni ya mjini ambapo watu wanaojiweza huenda kujivinjari katika mikahawa ya kifahari. Mwandishi anasema kuwa vijana hupitisha muda wao mwingi kwa starehe na anasa. Kwa mfano, katika *Baa ya Makaburini*, vijana huenda kujivinjari. Hata hivyo kuna ujambazi unaojiri na wateja wanaporwa mali. Semkwa anasema;

> *Tulibaki wachache pale, wakatukamata na kutuibia kila kitu, pesa, nguo, viatu hata na chupi... Uk. 39.*

Mtunzi amesawiri mandhari yanayoonyesha hali halisi katika jamii zetu hivyo yanaweza kuzua bibliotherapia. Visa vya ujambazi huwatia watu hofu na kusababisha fujo au ghasia kwa wanaopenda amani. Mfano, katika *Baa ya Makaburini,* ujambazi ulisababisha mtafaruku.

> *….meza anguka, viti vunjika. Gilasi anguka na sahani anguka. Ghafla bin vuu taa zikazima… Uk. 39.*

Hii ni hali halisi katika jamii.Wanafunzi wanaposoma hadithi hii wanaweza kujihusisha na mandhari haya. Vilevile, katika hadithi fupi ya *Shaka ya Mambo* katika diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine,* mwandishi amesawiri mandhari ya jijini Nairobi. Usafiri wa hapa jijini huwa ni kwa matatu. Katika jiji hilo kuna uwanja wa ndege wa kimataifa Jomo Kenyatta na majumba ya starehe. Taswira ya mandhari haya ni halisi. Kuna wanafunzi wanaoishi jijini Nairobi hivyo wao hujihusisha na mandhari haya kuweza kuzua BB. Mandhari haya yanaaminika.

Katika hadithi fupi ya *Siku ya Mganga* katika diwani ya *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine,* mandhari ya jijini Nairobi yamesawiriwa na Mwaibale anapowatembelea wateja wake jijini. Hakuacha kushangazwa na maendeleo ya kiteknolojia aliyoyaona katika nyumba za wateja wake alipoenda mjini kuwahudumia. Tofauti za kimaendeleo alizoziona ni pamoja na vitu kama runinga na majokofu. Cha muhimu katika hadithi hii ni mazungumzo ya watu wa mjini kuhusu ugonjwa mpya hatari ambao unaua watu. Mwandishi anasema hivi kuhusu Mwaibale;

> *Na kila alipofika huko, alikuwa haishi kushangazwa na maendeleo ya waliokuwa wakiishi mjini. Ndio alikuwa haishi kushangazwa na sanduku la picha za sinema lililokuwa kwenye kila sebule ya wateja wake ambalo hata watoto wadogo walikuwa wanaweza kuliwasha.*
> *…..Alikuwa haishi kushangazwa na makabati ya baridi… Uk. 23*

Mandhari anayosawiri mwandishi ni hali halisi katika maisha ya mjini. Wakazi wengi wana televisheni na majokofu. Mandhari haya yanaaminika kwa wanafunzi kwani wengine wao huishi maeneo ya mjini. Hivyo, wanapoisoma hadithi ya *Siku ya Mganga,* watajihusisha na yale mazingira ambayo wameyazoea. Katika hadithi ya *Hekima za Wajinga* katika diwani ya *Kiti cha Moyoni na Hadithi Nyingine,* mwandishi amesawiri mandhari ya jiji la Nairobi. Mama mtu anafunga safari kutoka Kimilili kuja kumtembelea mwanawe jijini Nairobi.

**h) Mandhari ya Nyumbani na BB**

Katika hadithi fupi ya *Shogake Dada ana Ndevu* katika diwani ya *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine,* mandhari yalikuwa ya nyumbani kwao Safia ambaye alikuwa mwanafunzi wa darasa la nane akijiandaa kwa mtihani. Safia anamwalika Kimwana kudurusu vitabu nyumbani kwao kumbe alikuwa mpenziwe. Haya yote yanatendeka nyumbani kwao akina Safia. Mwandishi anasema;

> *Lakini wakati mrefu umepita tokea Safia kuomba ruhusa kwa wazazi wake kwamba alitaka kumleta kwao shoga Kimwana, aje adurusu naye masomo ili wajiweke tayari kwa mitihani yao migumu ya kuingia kidato cha kwanza Uk. 30.*

Mandhari haya ni ya hali halisi na yanaaminika hivyo yanaweza kutumika kwa bibliotherapia. Vilevile, katika hadithi fupi ya *Fumbo la Mwana katika diwani ya Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine,* mwanzoni mwa hadithi mandhari ni nyumbani kwake mzee Atanasi babake Nanda. Mwandishi anasema;

> *Mzee Atanasi alikuwa katulia chini ya mpapai uliopo mbele ya nyumba yake. Kiti chake cha henzirani kimegusa kidogo shina la mti huo,*

*mguu wake wa kulia kaupachika juu ya ule wa kushoto. Anasinzia... Pana kopo lenye mabaki ya uji wa mtama ….Uk. 90*

Nanda anarejea kutoka shuleni na barua kutoka kwa mwalimu mkuu ikimtaka babake aende kumwona mwalimu huyo. Mandhari haya yanaonyesha vile vile kuwa ni mazingira ya kijijini na wakazi wa hapa kama mzee Atanasi ni wakulima. Mandhari katika hadithi fupi husaidia mwandishi kuibuka na maudhui husika.

Katika hadithi ya *Hekima ya Wajinga* katika diwani ya *Kiti cha Moyoni na Hadithi Nyingine*, mwandishi amesawiri mandhari ya nyumbani kwake Japheth Makata katika mtaa wa Lavington jijini Nairobi. Mwandishi anasema;

*Walifika mtaa wa Lavington- mtaa wa walalahai-usiku baada ya jua kuzama upande wa magharibi. Mwangaza wa jua uliupisha mwangaza wa mataa ya umeme… Uk. 62.*

Mandhari haya yanasawiri hali halisi ya maisha. Mji wa Lavington ni wa kifahari.
Langoni pa kasri la Makata palikuwa na mlalahoi mmoja aliyekuwa bawabu pale.
Mandhari ya hadithi hii yanaaminika hivyo kuweza kuzua BB.

Katika hadithi fupi ya *Mayai Waziri wa Maradhi* katika diwani ya *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine*, mwandishi amesawiri mandhari ya nyumbani. Tunamwona mhusika Mayai Waziri wa Maradhi akiwa ametulia nyumbani mwake. Mwandishi anasema;

*…alikuwa amekaa peke yake nyumbani akitazama buku kubwa la picha alizopigwa za zamani na sasa. Mkewe ambaye aligombana naye alikuwa ametoroka siku chache zilizopita. Uk. 63*

Mandhari ya hadithi fupi yanatuonyesha jinsi mwandishi alitumia mbinu rejeshi kutukumbusha hali ya Mayai Waziri wa Maradhi ilivyokuwa awali kabla ya kupata cheo. Vilevile katika hadithi ya *Ngome ya Nafsi* katika diwani ya *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine*, mandhari ya nyumbani yamejitokeza wakati Naseko anakumbuka jinsi watu asiowajua walifika pale nyumbani kuongea na wazazi wake. Naseko anasema;

*Alielewa kwa nini ng'ombe na mbuzi walikuwa wakiletwa kwao jioni jioni na watu asiowafahamu...Uk. 105*

Wazazi wake Naseko walikuwa wamemwoza kwa mzee Sakaja na wakapokea mahari. Katika hadithi fupi ya *Shamba la Miwa katika diwani ya Kiti cha Moyoni na Hadithi Nyingine*, mwandishi amesawiri mandhari ya nyumbani. Hadithi inapoanza, Kutosi Wesisi alikuwa katika nyumba yake. Alikuwa anatalii mali anayomiliki. Mwandishi anasema;

*Alikuwa kwenye ushoroba wa nyumba yake anatalii daftari lake la rasilmali anayomiliki. Alitazama taarifa ya akaunti zake kwenye benki….trekta mbili...nyumba za kupanga Bungoma..Uk. 97*

Kutosi Wesisi alikuwa tajiri wa kutajika pale mjini Bungoma. Aliendeleza kilimo biashara aina nyingi. Mandhari haya yaliangazia hali halisi ya maisha katika jamii. Mandhari haya ni ya kibibliotherapia.

**i) Mandhari ya Maabadani na BB**

Mandhari ya maabudu yamesawiriwa katika hadithi teule. Katika hadithi ya *Pwaguzi* katika diwani ya *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine*, kuna mandhari ya dini ya Kiislamu. Hadithi hii inasimulia ulaghai unaotekelezwa na Salim na Shehe Kijuba ambao ni wahusika wakuu katika hadithi hii. Salim alikaribishwa kwa mikono miwili hasa kwa kujitolea kutoa mafunzo ya kidini pale msikitini na kuwafunza vijana michezo. Aliwadanganya vijana kuchanga pesa kidogo ili wazitumie kununua vifaa walivyohitaji. Anasema;

*Aliwaambia wachange kiasi kidogo cha pesa naye atakapoenda kwao kuvuna mashamba yake, atawaongezea pesa ili awaletee vifaa Walivyohitaji… Uk. 53.*

Hadithi fupi ya *Msamaria Mwema katika diwani* ya *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine*. Ilikuwa siku ya Jumapili. Likono alikuwa mbioni akitoka kanisani. Mwandishi anasema;

*Akilini alikuwa akiyachefua mafundisho ya leo kanisani alikokwenda kwa ajili ya chakula cha kiroho… Uk. 78*

Mandhari ya asubuhi huangazia hali halisi katika jamii kwa hivyo inaweza kutumiwa kwa bibliotherapia.

**MAHITIMISHO**

Matokeo yalionyesha kwamba bibliotherapia hujitokeza katika mandhari yanayosawiriwa katika

diwani hizi za hadithi fupi teule. Mandhari yaliaminika katika hali halisi ya maisha ya wanafunzi wa shule za upili. Mandhari ya shuleni, nyumbani, mashambani na hata mjini yalisawiri hali halisi katika maisha ya wanafunzi. Matokeo kuhusu mandhari katika hadithi fupi teule yalionyesha umuhimu wake katika kuathiri tabia ya mwanafunzi vile inavyoathiri sifa na tabia za mhusika. Kufaulu kwa bibliotherapia hutegemea pakubwa ikiwa mwanafunzi anaweza kutagusana na mandhari katika hadithi fupi teule. Mandhari huweza kuibua sifa na tabia za wahusika na maudhui katika hadithi fupi za fasihi ya Kiswahili katika shule za upili, hivyo hufanikisha bibliotherapia kwa wanafunzi. Hata hivyo, mandhari ya sehemu za vilabuni na danguroni kama vile katika hadithi za *Nipe Nikupe*, *Samaki wa Nchi za Joto na Gilasi ya Mwisho Makaburini* huenda zisitimize bibliotherapia kwa wanafunzi kwa vile mandhari yanayosawiriwa pale hayawafunzi wanafunzi maadili.

**MAREJELEO**


Carlisle, A. (2000). Reading logs: An application of reader response theory in ELT. *ELT Journal*, 54(1), 12-19.

Chokocho, A. na Kayanda, D. (2016). *(Mha): Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine.* Longhorn Publishers.

Habwe, J. (2010). (Mha) Mizungu ya Manabii na Hadithi Nyingine. Phoenix Publishers.

Kang'eri, S. N. (2017). Uchunguzi wa Vipengele Teule vya Fani katika Riwaya ya Mashetani wa Alepo. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Katutu, R. (2013). *Mtindo katika Diwani ya Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine*. Tasnifu ya uzamili Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Kavanaugh, C. A., & Fiorini, J. J. (2009). Uses of Bibliotherapy for adoptive children and their families. Paper presented in *The American Counseling Association Annual Conference and Exposition*, Charlotte, NC.

Maich, K., & Kean. S. (2004). Read two books and write me in the Morning: Bibliotherapy for Social Emotional Intervention in the inclusive Classroom. In *Teaching Exceptional Children Plus*.

Mathai, M. (1983). *Bibliotherapy: It's Potential in Kenyan Prisons*. Unpublished Masters Thesis Kenyatta. University Kenya.

McOnyango, O. (2006). *Mimba Ingali Mimba na Hadithi Nyingine*. Focus Publishers.

Mohochi, E. (1995). *Fani katika hadithi fupi*. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Muusya, J. K. (2012). Mandhari katika Hadithi Fupi: Ulinganishaji wa *Diwani za Pendo la Heba na Hadithi Nyingine* na *Mizungu ya Manabii na Hadithi Nyingine*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Njogu, K., na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi Nadharia na Mbinu*. Jomo Kenyatta Foundation.

Ongarora, S. (2007). Mtindo katika Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Rosenblatt, L. (1978). *The Reader, The text, The poem: The Transactional Theory of the Literary Work.* Southern Illinois Press.

Rosenblatt, L. (1995). *Literature as Exploration*. The Modern Language Association of American. (5th Edition).

Wamitila, K. W. (2002). *Kamusi ya Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake.* Nairobi: Phoenix Publishers.

Wamitila, K. W. (2003). Kamusi ya Fasihi: Misingi. Istilahi na Nadharia Nairobi: Focus Publication.